# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na nguvu, tukaweza kukutana hapa leo hii, katika Chombo hiki muhimu cha nchi yetu, kwa lengo la kuwawakilisha wananchi wetu wa Zanzibar. Ninamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza letu hili, kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa uweledi na umahiri mkubwa, namuaomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara ili tuweze kufikia malengo na wajibu wetu katika chombo hiki adhimu na muhimu kwa nchi yetu.

Vile vile, tunatoa pongezi za kipekee kwa Uongozi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa ushirikiano wanaotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawataka waongeze ushirikiano huo

pamoja na bidii na ari katika kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upekee kabisa nawashukuru Wajumbe wezangu wa wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kutoa katika kutekeleza kazi za Kamati na hatimae tukaweza kuwasilisha hotuba hii kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2026/2027 mbele ya Baraza letu Tukufu, kama takwa la Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni zetu za kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024 linavotaka uwasilishaji wa maoni ya Kamati kuhusiana na Makadirio ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati walioshiriki hadi kukamiliki ripoti hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Dkt Mohamed Ali Suleiman | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdulghani Ismail Zubeir | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Said Ali Juma | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Moza Mohamed Khamis | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Juma Usonge Juma | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Said Azana Hassan | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| *9.* | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| *10.* | Ndg. Hafidh Ussi Haji | Afisa wa Bajeti |

MAKUSANYO YA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** nianze kuwasilisha maoni ya uchambuzi wa Kamati kwa kuagalia suala la Makusanyo ya Mapato ambapo kwa masikitiko makubwa, Kamati imebaini kwamba Wizara imekumbana na changamoto kadhaa, zilizosababisha mapungufu ya makusanyo ya mapato ambapo hadi kufikia Mwezi Machi 2026, Wizara imekusanya **Tzs Bilioni 1.94** sawa na asilimia 45 tu ya makadirio, ambayo ni **Tzs Bilioni 3.51.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeshtushwa na hali hii, ambapo baada ya mahojiano na watendaji wa Wizara tumebaini kwamba, malengo ya ukusanyaji hayakufikiwa kutokana na Taasisi zinazotoa Leseni na Tozo kutowasilisha michango yao kwa Mamlaka ya Udhibiti na Utoaji wa Leseni. Pia, Kamati imebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Serikali zimeshindwa kulipa ada ya ukodishwaji wa vifaa na ukumbi katika eneo la maonesho Dimani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazitaka Taasisi zote zinazopaswa kupeleka michango yao kwa Mamlaka ya Udhibiti na Utoaji wa leseni na zile zinazopata huduma katika eneo la maonesho Dimani kulipia madeni yao, huku pia tukiwahimiza watendaji wa Wizara kuongeza juhudi za kufuatilia kikamilifu madeni hayo ili hatimae katika robo ya mwisho iliyobakia kupata mapato zaidi yatakayosaidia kuinua makusanyo ya Wizara.

**Mheshimia Spika,** katika hatua nyengine, Kamati inawashauri wakadiriaji wa Mapato kutoka Wizara ya Fedha kukaa pamoja na watendaji wa Wizara husika wakati wa ukadiriaji wa mapato ili makadirio yanayopendekezwa

yaende sambamba na uwezo wa taasisi zinazokadiriwa. Kamati inatoa mfano wa Makadirio ya Wizara hii, yanakwenda kupungua kutoka **Tzs Bilioni 3.5** mwaka 2025/2026 na kushuka hadi **Tzs Bilioni 3.0** kwa makisio ya Mwaka 2026/2027 kutokana na sababu ile ya changamoto ya kutokufikia malengo ya ukusanyaji kwa mwaka huu.

## MIRADI INAYOSIMIWA NA WIZARA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuthamini hatua inayoendelea kufikiwa katika utekezaji wa Miradi ya Wizara ambayo ni Mradi wa kuanzisha na Kuendeleza Maeneo ya Viwanda, Mradi wa kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar, na Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhika na suala la uiingizwaji wa Fedha kutoka Serikalini katika Miradi ambayo imeingiziwa fedha chini ya asilimia 28. Kamati yetu imebaini kwamba kasoro hii ni sehemu ya Changamoto zinayoikumba Wizara hii na kupelekea miradi hiyo kutokamilika kwa wakati. Kamati inaiomba Serikali kuwaiingiza fedha zote, na kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza na kuikamilisha miradi hiyo kama walivyojipangia.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati inapitia utekelezaji wa Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, tulishawishika na utekelezaji wa Huduma na Shughuli za Programu hii ikiwemo ukamilishwaji wa uandaaji wa Sera ya Milki Bunifu. Kamati inaamini utekelezaji wa kerá hii utasaidia katika utambuzi na ulinzi wa kisheria katika sekta hii ya Milki Bunifu. Wakati huo huo Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara (BPRA) kuongeza bidii kutoa taaluma kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa kusajili Milki Bunifu ili jambo hili liweze kufahamika vyema katika jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha **Tzs Bilioni 4.63** zilizoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii, ili kuiwezesha Wizara kuimarisha mazingira ya ufanyaji wa biashara na huduma kwa kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni, kuimarisha mifumo ya Tehama, Usajili wa Mali na Biashara.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, Miongoni mwa jukumu la Wizara ni Uhamasishaji wa Viwanda kuhamia katika eneo la viwanda ili kupunguza changamoto zinazojitokeza pindi uwekezaji wa viwanda unapofanyika katika maeneo ya makaazi ya watu. Kamati inaielekeza Wizara kuendelea na uhamasishaji huu kwani tunafahamu kwamba maeneo hayo ya Viwanda tayari serikali imewekeza fedha nyingi ili kuimarisha

miundombinu yote muhimu na kurahisisha shughuli za viwanda na uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu mtekelezaji mkuu wa Programu hii ni Idara ya Maendeleo ya Viwanda, ambayo miongoni mwa majukumu yake ni kufanya vikao na Wadau wa Sekta ya Viwanda kwa ajili ya kubaini vikwazo vinavyiikabili sekta hiyo na kuvipatia ufumbuzi. Katika kufuatilia utekelezaji wa jukumu hilo, Kamati ilitembelea baadhi ya viwanda kikiwemo Kiwanda cha Unga wa Ngano (fly Fox) Finya, Kiwanda cha Maji Water Com Kinyikani na Kiwanda cha Maji cha Lulu Chamanangwe Pemba. Kamati imebaini kuwa, licha ya viwanda hivyo kusaidia katika kutoa ajira kwa jamii lakini vinakabiliwa na changamoto kadhaa zinazokwaza maendeleo mazuri ya viwanda hivyo ikiwemo;-

a) Umeme mdogo ambao pia mara kwa mara unakatika na kupelekea kuharibika kwa vifaa.
b) Utitiri wa Kodi,
c) Usafirishaji wa mali ghafi za uzalishaji na bidhaa zinazozalishwa kutoka nje ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwasidia wawekezezaji hawa wazalendo katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili ili waweze kutekeleza malengo yao ya kuongeza uzalishaji, kuzalisha nafasi za ajira, na kuchochea ukuaji wa pato la Taifa.

Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwekeza katika será na miundombinu imara

itakayowarahisishia wawekezaji katika sekta ya Viwanda ikiwemo upatikanaji wa malighafi na masoko ili kuepusha viwanda hivyo kusistisha shughuli zao muda mfupi tu baada ya kuanza uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwengine , Kamati imeshtushwa na taarifa za Idara ya Maendelea ya Viwanda kuhusiana na rasilimali watu ya Idara hii ambapo hadi tunapitia makadirio haya, Idara hiyo ina jumla ya wafanyakazi 14 tu, Unguja wakiwa ni 13 na Kwa upande wa Pemba ni mmoja (1) tu. Kamati inajiuliza wakati nchi yetu inahimiza maendeleo ya viwanda tutakwendaje na wafanyakazi hawa 14?. Tutakwendaje kuifungua Pemba katika Sekta ya Viwanda ikiwa kuna mtumishi mmoja tu katika Idara ya Maendeleo ya Viwanda?. Kamati inamuomba Mhe Waziri kuja na tarifa za kulitosheleza Baraza lako tukufu kuhusiana na kadhia hii ya upungufu mkubwa wa watumishi katika Idara hii.

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika**, katika Programu Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara yenye lengo la kukuza masoko kwa bidhaa za Zanzibar, Kamati inajikita zaidi kwa Wakala wa Vipimo (ZAWEMA), taasisi ambayo inajukumu la kuhakikisha majibu ya vipimo katika muamala wa biashara yanakua huru na haki kwa lengo la kumlinda mtumiaji.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mahojiano na watendaji wa taasisi hii, Kamati imebaini changamoto kadhaa zinazokwaza utendaji wao wa kazi ikiwemo ruzuku kutoka serikalini, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2026 ZAWEMA imepatiwa asilimia **23.24%** tu ya ruzuku ya bajeti iliyotengwa.

Aidha, ZAWEMA inakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi pamoja na changamoto nyengine zinazoathiri uendeshaji na ukusanyaji wa mapato. Utafiti wa Kamati umebaini kwamba, changamoto nyingi zinazoibuka katika utendaji wa ZAWEMA zinatokana na mchakato unaoendelea kuhusiana na kuunganishwa baina ya Taasisi hiyo na Taasisi ya Viwango (ZBS).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Serikali kuangalia vyema uwepo wa Taasisi hii ya ZAWEMA kutokana na majukumu yake ambayo ni muhimu katika mnyororo mzima wa biashara hapa nchini kama inavyofanyika duniani kote. Mheshimiwa Spika, kabla ya kupitia Fungu la Wizara hii, Kamati ilibahatika kutembelea Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) na kushuhudia maendeleo makubwa yaliyofikiwa na taasisi hiyo. Hapa tunaiomba Wizara kwenda kujifunza na kuona kwa jinsi gani na sisi tunaweza kuimarisha Taasisi yetu ya ZAWEMA ili kuendena na kasi ya serikali kwenye uwekezaji wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Kamati yetu inaafiki vipaumbele vyote vilivyopangwa na Taasisi hii ikiwemo uendelezaji wa maabara zake zote kama zilivyoainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri . Aidha Kamati kamati inatoa wito wa Kupatiwa msaada wa fedha za kujengewa jengo jengine la Maabara (Test House) katika eneo la Dunga na Ofisi na Maabara Chamanagwe Pemba pamoja na kupatiwa ruhusa ya nafasi za uajiri wa wafanyakazi ili kuongeza ufanisi na utendaji wa kazi za upimaji maabara na ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inamalizia maoni yake ya Bajeti kwa Wizara hii kwa kuangalia Shirika la Biashara la Zanzibar (ZSTC) na zao la Karafuu. Kamati inatambua umuhimu wa zao la Karafuu kama urithi wa kiuchumi na kihistoria kwa Zanzibar. Hivyo Kamati, inakubaliana na mipango yote ya Serikali inayokusudiwa kutekelezwa na ZSTC kama alivyokwisha kuelezwa na Mheshimiwa waziri, ikiwemo ununuzi wa karafuu na makonyo, uzalishaji wa mafuta ya mimimea na ujenzi wa maghala. Kamati inaamini kwamba, hatua hizo zinalenga kuhakikisha Kilimo cha Karafuu kinaendelea kuwa miongoni mwa chanzo cha ajira, kipato na maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, wakati wa kazi za kamati, Kamati yetu ilipofanya mahojiano na Watendaji wa ZSTC na ilibaini changamoto zifuatazo;-

a) Uchelewaji wa meli za kusafirishia karafuu zinazokwenda nnje ya nchi, hasa kwa upande wa Pemba,
b) Kushuka kwa bei ya kuuzia karafuu katika soko la Dunia,
c) Kuwa na bakaa ya makonyo kwa kiasi kikubwa na
d) Kukatwa kwa mikarafuu kwa ajili ya kupisha miradi mingine ya kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inashauri kuchukuliwa kwa juhudi za makusudi za utatuzi wa changamoto hizo, ikiwemo kampeni maalum ya kuwahamasisha wananchi kupanda miche mipya ya mikarafuu ili kuchukuwa nafasi ya ile inayokatwa kwa sababu mbali mbali ikiwemo kuzeeka pamoja na kupisha miradi ya Maendeleo.

Pia, Kamati inasisitiza suala la uaminifu hasa katika kuweka madaraja ya karafuu *Grading* ili kuleta imani kwa wakulima wanaokwenda kuuza karafuu katika Shirika hilo. Aidha, Kamati inaiomba Wizara kupitia Shirika lake la ZSTC kuwasaidia kitauluma wakulima wetu hasa katika suala la upandaji wa mikarafuu itakayoweza kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba hii kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifuatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza Mipango aliyojipangia.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

………………………………………

**(Mhe: Dkt Mohammed Ali Suleiman).**
**Makamu Mwenyekiti,**
**Kamati ya Utali, Buashara na Kilimo,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**